# Misingi ya Kitheolojia: Mwongozo wa Kozi

**Imani ya Mitume**
**Kujenga Theolojia Binafsi**

**Maelezo ya Kozi**

Kwa muda wa takribani milenia mbili sasa, kumekuwa na imani ya pamoja miongoni mwa Wakristo ambayo imewekwa kwa muhtasari katika Imani ya Mitume. Wakati huo huo, theolojia ya mrengo wa kiinjili ya kisasa imegubikwa na mitazamo tofauti inayokinzana. Tofauti nyingi zinatokea baina ya madhehebu, na zingine zikitokea kati ya madhehebu na makanisa binafsi. Pamoja na tofauti nyingi za kimitazamo inayoshindana kwa ajili ya utii wetu, je, wafuasi wa Yesu watawezaje kujua nini cha kuamini? Ni jinsi gani tupaswa kujidhatiti katika mafundisho mahususi pamoja na mapokeo?

Kozi hii itakusaidia kutafakari maswali haya muhimu na mengine mengi. Msingi wa kozi hii upo katika video mbili zilizoandaliwa na Huduma ya Third millennium, yaani: *Imani ya Mitume, na Kujenga Theolojia Binafsi*, itaongozwa na Dkt. Van Gayton na Dkt. Vincent Bakote pamoja na michango mingine kutoka kwa maprofesa mbalimbali.

**MALENGO YA KOZI, MAKUSUDI NA ORODHA YA MODULI**

**Malengo:**

Katika kozi hii, tunapenda kujifunza mambo yafuatayo:-

1. Tunatarajia utajifunza sababu muhimu za historia ya Imani ya Mitume na pia utajifunza maana ya kila mafundisho yaliyotajwa katika Imani ya Mitume.
2. Tunaamini utashawishika kujua thamani ya Imani ya Mitume na faida zake kwaajili ya makanisa ya kisasa, na kuamini mafundisho yaliyopo ndani yake.
3. Tunaamini kuwa utayatumia mafundisho ya kozi hii katika moyo wako na maisha yako, kumuamini mungu kuwa baba yako, kumwamini Yesu kama mwakozi wako, kumwamini Roho Mtakatifu kama kiongozi wako, kuishi kwa neema na kushiriki katika shughuli za kikanisa.
4. Tunaamini utajifunza asili halisi na lengo la theolojia.
5. Tunaamini utaipenda theolojia kwa upya, na kuwa utavutiwa kuhusu kufanya theolojia ambayo inafuata maandiko na itakayobadilisha moyo wako na maisha yako.
6. Tunaamini utafanya mabadiliko katika maisha yako kama jibu la mafundisho haya. Kozi hii lazima ibadilishe namna unavyofanya theolojia na kuchambua

theolojia kwa kuzingatia vipengele vya othodoksia, othopraksia, na othopatosia.

**Makusudi.**

Kwa kutimiza mambo yafuatayo, ni ishara kuwa malengo ya kozi yametimia;

1. Kupata madaraja yanayoridhisha katika majaribio na mitihani ya kozi, na kudhihirisha kuwa unaweza.
    - Kutambua taarifa muhimu kuhusu historia ya Imani ya Mitume.
    - Kutambua maana ya mafundisho yaliyoelezwa katika Imani ya Mitume.
    - Kutambua maana ya mafundisho yaliyoelezewa katika Imani ya Mitume.
    - Kutambua sababu kuu ya kujifunza theolojia.
    - Kutofautisha umuhimu wa othodoksia, othopraksia, na othopatosia katika jukumu la theolojia.
    - Kutofautisha aina mbalimbali za ufunuo pamoja na umuhimu wa kufanya theolojia.
    - Kutofautisha mitazamo mbalimbali ya misukumo na tafsiri sahihi ya maandiko.
    - Kutambua mitazamo mikuu tofauti ya marekebisho ya theolojia.

2. Kukamilisha miongozo ya kujifunza kozi hii, ukielezea mtazamo wako kuhusu Imani ya Mitume na mafundisho yake. Kuelezea uhusiano wako na Mungu baba, Yesu, pamoja na Roho Mtakatifu, na ukionesha kuwa unaishi kwa neema na kushiriki kwenye shughuli za kanisa. kuelezea mtazamo wako kuhusu theolojia ukionesha namna ulivyoyatumia mafundisho ya kozi hii katika maisha yako; pia utafanya theolojia na kuchambua maneno ya kitheolojia ukizingatia
maeneo ya othodoksia, othopraksia na othopatsia.

**Orodha ya Moduli kwa Kozi ya Misingi ya Kitheolojia**

1. Makala za Imani
2. Mungu Baba
3. Yesu Kristo
4. Roho Mtakatifu
5. Kanisa
6. Wokovu

7. Theolojia ni nini?
8. Kuchunguza Theolojia ya Kikristo
9. Kutegemea Ufunuo
10. Mamlaka Iliyopo katika Theolojia

**MAELEZO KUHUSU VIPENGELE VYA KOZI**

**Beji**

1. Kila juma katika mazungumzo yenu mtatenga muda kwaajili ya kufanyia kazi vipengele vya Beji. Mwongozo huu wenye kurasa mbili utampa mkufunzi wenu mwongozo wa jumla wa namna mnavyotakiwa kuendeleza ujuzi huu muhimu katika huduma.
2. Katika wiki chache za mwanzoni, tumia muda wako ukiwa na kundi lako pamoja na mkufunzi wako mkipitia mada za kujadili kwenye maelezo ya beji.
3. Baada ya kuweka msingi imara kupitia majadiliano ya kikundi, tumia wiki zilizobaki kuifanyia kazi beji (mambo ya kufanya).
4. Utapatiwa beji pale mkufunzi wako atakapojiridhisha kuwa umetimiza vigezo vya beji kwa mujibu wa maelekezo yake.

**Moduli**

1. Jifunze kwa kutazama video, kusikiliza sauti, au kusoma nukuu.
2. Kamilisha mwongozo wa kujifunza kwa kila somo. Miongozo ya kujifunza itakuandaa wewe kujibu maswali ya mitihani, mazoezi ya kwenye mitandao na kukusaidia kuyatumia mafundisho ya somo katika maisha yako binafsi.
3. Fanya mitihani ya kila somo, mitihani itatolewa na mkufunzi wako. Mitihani inaweza kurudiwa kama kuna ulazima, tunapendekeza ufikie alama zaidi ya asilimia 80% kabla ya kushiriki mjadala wa wiki na kuhakikisha kuwa umeelewa maneno kwa usahihi.
4. Shiriki katika majadiliano ya kila wiki kwenye kundi lako pamoja na mkufunzi wako, mkitumia miongozo kuhusu kozi na uwezo wa kutumia maneno kwa usahihi katika maisha yako au huduma yako. Tunapendekeza mijadala kupitia video isiwe chini ya lisaa limoja.

**Mtihani wa Mwisho**

Unaweza ukafanya majaribio zaidi ya mara moja kama unahitaji kujipima, lakini unatakiwa ujifunze na kusubiri kwa muda wa saa moja kabla ya kufanya jaribio jingine. Alama yako rasmi itakuwa ile uliyofanya vizuri zaidi kwenye majaribio yako na tunapendekeza upate zaidi ya 80% kabla ya kuendelea na kozi inayofuata.

**Alama za Ufaulu**

Daraja la mwisho la ufaulu litahesabiwa kama ifuatavyo:

1. Majaribio ya darasani yatakuwa na alama 30 kila moja.
2. Mtihani wa mwisho utakuwa na alama 100.
3. Ripoti ya beji ya maombi haiwezi kubadilisha daraja lako lakini ni lazima ipitishwe na mkufunzi ili uwe umekamilisha kozi.

*Alama za jumla katika kozi zinazozidi 80% zinahesabiwa kuwa ni ufaulu.*

**…………………………………………………..**

**<u>Walioshiriki Kuandaa Kozi hii</u>**

**Mch. Azar Ajaj** ni mkurugenzi wa mahusiano ya uma na ni mkufunzi katika chuo kikuu cha Nazareth evangelical college.

**Mchungaji, Dkt Humphrey Akogyeram** ni profesa wa chuo cha Good news theological seminary, Accra, Ghana.

**Dkt. M. B.** ni profesa wa chuo cha Bethlehemu college and seminary.

**Dkt. David R. R. Bauer** ni mshauri wa shule ya Biblical interpretation na Ralph Waldo beeson profesa wa Inductine bible studies.

**Dkt. Steve Blakemore** ni profesa msaidizi wa falsafa katika chuo cha Wesley Biblical seminary.

**Dkt. D.A. Carson** ni profesa wa tafiti kuhusu gano jipya katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity school na muazilishi wa Gospel Coalition.

**Dkt. Knox Chamblin** (1935 – 2012) alitumika kama profesa wa gano jipya katika chuo cha Reformed Theological Seminary.

**Dkt. Paul Chang** ni mchungaji kiongozi katika kanisa la Monmouth Chinese Christian Church in Middletown, New Jersey.

**Dkt. Blao Chen** ni mkurugenzi wa miradi ya Kichina katika Thirdmill.

**Dkt. Steve Curtis** ni mkurugenzi wa Timothy Two Projects International.

**Dkt. Andrew Davis** ni mchungaji kiongozi katika kanisa la First Baptist Church of Durham, NC and is Visiting Professor of Historical Theology at Southeastern Baptist Theological Seminary.

**Dkt. James K. Dew, Jr**. ni profesa msaidizi wa Historia ya mawazo na falsafa katika chuo cha Southeastern Baptist Theological Seminary.

**Dkt. Jeff Dryden** ni profesa wa mafunzo ya bibilia katika chuo cha Covenant College.

**Dkt. J. Ligon Duncan III** ni kansela na mkurugenzi wa Reformed Theological Seminary na John E. Richards ni profesa wa Systematic and Historical Theology.

**Dkt. Bruce L. Fields** ni mwenyekiti wa Biblical and Systematic Theology Department and Associate Professor of Biblical and Systematic Theology katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School.

**Dkt. John Frame** ni profesa wa Systematic Theology and Philosophy katika chuo cha Reformed Theological Seminary in Orlando, Florida.

**Dkt. Matt Friedeman** ni profesa wa uinjilisti na utume katika chuo cha Wesley Biblical Seminary.

**Rev. Hutch Garmany** ni mchungaji na mchungaji mwanzilishi wa Grace Community Trenton in Trenton, Georgia.

**Rev. Michael J. Glodo** ni profesa mwandamizi wa mafunzo ya kibibilia katika chuo cha Reformed Theological Seminary in Orlando, Florida.

**Dkt. Steve Harper** ni makamu- rais muanzilishi wa Florida Dunnam campus of Asbury Theological Seminary in Orlando, FL.

**Dkt. J. Scott Horrell** ni profesa wa mafunzo ya Theolojia katika chuo cha Dallas Theological Seminary.

**Rev. Clete Hux** ni mkurungenzi wa Counter-Cult Apologist at Apologetics Resource Center in Birmingham, AL.

**Dkt. Thaddeus J. James, Jr.** ni makamu wa rais wa taaluma katika chuo cha Birmingham Theological Seminary.

**Dkt. Dennis Johnson** ni mshauri wa taaluma na profesa wa Theolojia ya vitendo at Westminster Seminary California.

**Dkt. Keith Johnson** mkurugenzi wa elimu ya Theolojia kwaajili ya the U.S campus ministry of Campus Crusade for Christ and is a guest professor of Systematic Theology for Reformed Theological Seminary.

**Dkt. Jeffrey Jue** ni profesa wa historia ya kanisa katika chuo cha Westminster Theological Seminary.

**Dkt. Kelly M. Kapic** ni profesa wa mafunzo ya Theolojia katika chuo cha Covenant College.

**Dkt. Riad Kassis** ni mkurugenzi wa kimataifa na baraza la kimataifa wa Evangelical Theological Education.

**Dkt. Craig S. Keener** is the F.M. and Ada Thompson Chair of Biblical Studies at Asbury Theological Seminary.

**Dkt. Michael J. Kruger** ni rais na profesa wa agano jipya katika chuo cha New Testament at Reformed Theological Seminary in Charlotte, N.C

**Dkt. Dan Lacich** ni mchungaji katika kanisa la Northland, A Church Distributed in Orlando, FL.

**Dkt. Samuel Ling** ni muanzilishi wa China Horizon.

**Dkt. Robert G. Lister** ni profesa mwandamizi wa mafunzo ya kibibilia na Theolojia katika chuo cha Talbot School of Theology.

**Dkt. Jeff Lowman** ni mchungaji kiongozi wa Evangel Church PCA in Alabaster, Alabama and Professor of Homiletics and Systematic Theology at Birmingham Theological Seminary.

**Dkt. Scott Manor** ni profesa msaidizi wa theolojia ya kihistoria na makamu wa rais taaluma lakini pia ni mshauri wa kozi katika chuo cha Knox Theological Seminary.

**Rev. Dr. Emad A. Mikhail** ni rais wa Great Commission College in Egypt.

**Dtk. J. Gary Millar** ni mkuu wa chuo cha Queensland Theological College and Founding Council Member of The Gospel Coalition, Australia.